JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
Bodi ya Usajili wa Wathamini
Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
Mji wa Serikali Mtumba,Eneo la Mtumba, Mtaa wa Ardhi
S. L. P. 325, Dodoma, Tanzania
Simu Na: +255 733542654 Email. Registrar@vrb.go.tz

# TAARIFA KWA WATHAMINI WOTE WALIOKUWA WAMESAJILIWA CHINI YA SHERIA YA USAJILI WA WAPIMA ARDHI (SURVEYORS REGISTRATION ACT, CAP. 270)

Bodi inapenda kuwajulisha Wathamini wote waliosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wapima Ardhi (Sura. 270) kabla ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya 2016, Sura. 138 kuwa, imetoa siku tisini (90) kuanzia tarehe ya tangazo hili, kuwasilisha maombi ya kuhuisha usajili kulingana na masharti ya kifungu cha 73 (Savings and Transition Provisions) cha sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Sura 138.

Hatua zinazohitajika ni pamoja na kuwasilisha maombi ya usajili kwa Msajili kupitia fomu ya maombi ikiambatanishwa na nakala ya Cheti cha Usajili chini ya **National Council of Professional Surveyors (NCPS),** maelezo ya sababu za kuchelewa kuomba awali kama ilivyokuwa imeelekezwa na viambatisho vya kuthibitisha maelezo hayo.

Fomu ya maombi inapatikana kwenye tovuti ya Bodi www.vrb.go.tz. Kwa ufafanuzi zaidi, mawasiliano yafanyike kupitia barua pepe registrar@vrb.go.tz au simu 0733542654.

**Kufanya uthamini bila usajili halali ni kosa chini ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Sura 138.**

**MSAJILI**

**06/03/2026**